# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 7*

### JE! WATOTO WABATIZWE?

Baadhi ya watu wa siku zetu wanaamini kwamba watoto hurithi dhambi za baba zao (yaani, dhambi za asili). Kwa hiyo, watu hawa huamuru hata watoto wachanga wabatizwe. Wala si ajabu, maana katika Biblia imo mistari fulani ambayo mtu anaweza kuisoma bila kuelewa maana yake. Tutachunguza baadhi ya mistari hii hapo mbele. Lakini kwanza tukumbuke jambo moja lililo muhimu.

Jambo hili ni kwamba, kwa kazi ya Shetani, hata mtu asiye na dhambi anaweza kuteswa katika hali ya kimwili. Tangu zamani watu wameelewa vibaya mambo kama haya wakidhani kwamba mwenye haki huteswa kwa sababu amerithi dhambi. Kwa mfano, twasoma:

"*Hata* (Yesu) *alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu? Yesu akajibu, Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake.*" Yohana 9:1-3

1. Kwa sababu mtu huyu alizaliwa kipofu, wanafunzi walifikiri amerithi dhambi ya nani? ___________________

2. Je! Yesu alikubali kwamba kipofu amerithi dhambi? ___________________

Hata katika siku za nabii Ezekieli baadhi ya watu walishindwa kuelewa kwamba watoto hawarithi dhambi. Kwa hiyo, walitunga mithali wakisema, "Baba wamekula zabibu mbichi, nao watoto (wasiokula) wakatiwa ganzi la meno." Ebu! tuone ikiwa Mungu alifurahi na usemi huu. Nabii Ezekieli alisema:

"*Neno la Bwana likanijia tena, kusema, Je! maana yake ni nini hata mkatumia mithali hii katika Israeli, mkisema, Baba wamnekula zabibu mbichi, nao watoto wakatiwa ganzi la meno? Kama mimi niishivyo, asema Bwana Mungu, hamtakuwa na sababu ya kuitumia tena mithali hii katika Israeli. Tazama, roho zote ni mali yangu; kama vile roho ya baba ni mali yangu, ndivyo ilivyo roho ya mwana mali yangu, <u>roho ile itendayo dhambi itakufa.</u>*" Ezekieli 18:1-4

3. Maana ya mithali ya Waisraeli ni kwamba wana hurithi dhambi za baba zao. Je! Mungu alifurahi na mithali hii? ___________________

4. Roho ya baba na ya mwana pia ni mali ya nani? ___________________

5. Roho gani itakufa? ___________________

"(Mwenye dhambi) *akizaa mwana, naye ameona dhambi zote za baba yake alizozitenda, akaogopa, asifanye neno lo lote kama hayo… naye amezifanya hukumu zangu, na kuzifuata sheria zangu; hatakufa huyu kwa sababu ya uovu wa baba yake, hakika ataishi… Lakini ninyi mwasema, Kwani yule mwana asiuchukue uovu wa baba yake? Yule mwana atakapofanya yaliyo halali na haki, na kuzishika amri zangu na kuzitenda hakika ataishi*." Ezekieli 18:14,17,19

6. Ingawa baba ni mwovu, je! mwana akiwa mwema atakufa kwa sababu ya uovu wa baba yake? ___________________

"*Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa;* *mwana hatauchukua uovu wa baba yake*, *wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe; haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake… Lakini nyumba ya Israeli husema, Njia ya Bwana si sawa. Ee nyumba ya israeli, je! njia zangu sizo zilizo sawa? njia zenu sizo zisizo sawa? Basi, nitawahukumu ninyi, nyumba ya Israeli, kila mmoja kwa kadiri ya njia zake, asema Bwana Mungu.*" Ezekieli 18:20,29-30

7. Je! maneno hayo ya Mungu yaonyesha ya kuwa watoto wanarithi dhambi? ___________________

8. Mungu amesema kwamba mwana hatauchukua nini? ___________________

9. Haki yake mwenye haki itakuwa juu ya nani? ___________________

10. Uovu wake mwenye uovu utakuwa juu ya nani? ___________________

11. Wanadamu wamesema kwamba njia za Mungu si nini? ___________________

12. Mungu atamhukumu kila mwanadamu kwa kadiri ya nini? ___________________

Mwanafunzi akiichunguza Biblia, ataona kwamba maneno yale "dhambi ya asili" hayajawahi kuandikwa katika Biblia. La! bali maneno hayo yametungwa na watu ambao wamekosa kuelewa mafundisho ya Biblia, Maana, hata katika Torati, Mungu alimwamuru Musa akisema:

"*Mababa wasiuawe kwa ajili ya watoto wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya baba zao; kila mtu na auawe kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe.*" Kumbukumbu 24:16

13. Mungu aliamuru watoto wasiuawe kwa ajili ya nani? ___________________

14. Kila mtu na auawe kwa ajili ya dhambi ya nani? ___________________

Watu wamekosa kuelewa kuhusu, kurithi dhambi kwa sababu wameshindwa kuelewa mstari unaoandikwa huko chini. Usome mstari huu kwa uangalifu mwingi ukikumbuka kwamba Mungu (ambaye hawezi kusema uongo) amesema "mwana hatauchukua uovu wa baba yake."

"*… mimi Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, nawapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao na kuzishika amri zangu.*" Kumbukumbu 5:9-10

15. Je! wana wale wanaopata uovu wa baba zao ni wana wanaompenda Mungu au wanaomchukia? ___________________

16. Je! wana hawa hupata uovu wa baba zao kwa sababu wameurithi au kwa sababu wao nao ni waovu? ___________________

17. Je! wana wale ambao wanampenda Mungu na kushika amri zake hupata uovu wa baba zao au hupata rehema? ___________________

**DHAMBI YA ADAMU NA KIFO CHA KIMWILI**

Watu wengine wanaweza kubisha wakiuliza kwamba ikiwa watoto hawarithi dhambi, basi kwa nini wanakufa? Ingawa mtoto harithi dhambi za baba yake, walakini mara nyingi anaweza kuteswa (katika hali ya kimwili tu) kwa sababu ya kosa la baba. Kwa mfano, baba akiwa mwizi, mtoto wake anaweza kufukuzwa na watu na kutukanwa ingawa mtoto mwenyewe ni mwema. Tena, baba ambaye amelewa pombe, akikanyagwa na gari hali amembeba mtoto wake, basi mtoto naye anaweza kufa. Ingawa watoto hawa wameteswa katika hali ya kimwili, walakini katika hali ya kiroho Mungu hawezi kuwahesabu kuwa wenye dhambi. Kumbuka jinsi mambo mengi mabaya yalivyompata Ayubu hata ingawa Ayubu mwenyewe alikuwa mwema (Ayubu 1:7-22; 2:3-10).

Kifo cha kimwili hakionyeshi kwamba mtu ni mwenye dhambi. La! maana hata watu wenye haki waliobatizwa hufa! Basi, kwa nini hata wenye haki hufa? Wenye haki nao hufa kwa sababu wamerithi mwili wa Adamu ingawa hawarithi dhambi zake. Tutoe mfano:

Hapo zamani watu 20 walipanda gari la basi wakitaka kusafiri. Usiku, watu wote walipokuwa wakilala usingizi, dreva akakosa sheria akagonga gari jingine. Watu wote waliokuwamo ndani ya basi wakaumia vibaya. Polisi wakaitwa wakaanza kupeleleza wakahakikisha kwamba mwenye kosa alikuwa dreva wa basi. Kwa hiyo, dreva huyo akachukuliwa mbele ya hakimu na, hata ingawa alikuwa na maumivu, akapewa adhabu pia.

Je! mfano huu maana yake nini? Dreva wa basi ni Adamu na basi lenyewe ni mwili wake Adamu. Waliopanda basi ni sisi sote tuliozaliwa kwake. Tulikuwa kama tumelala maana tulikuwa hatujazaliwa bado Adamu alipotenda dhambi. Hivyo, alipokosa Adamu akaumia pamoja na sisi pia (maana tumerithi mwili wake unaokufa). Walakini, mwenye kusimama mbele ya Mungu aliye hakimu atakuwa Adamu tu aliyekuwa na hatia. Ingawa miili yetu hufa kwa sababu ya Adamu, walakini roho zetu hazina hatia yake.

Watu wengi wamekosa kuelewa jambo hili kwa sababu ya maneno ya Paulo yaliyoandikwa katika Warumi 5. Lakini kabla hatujaangalia maneno yake, inafaa tukumbuke onyo la mtume Petro jinsi alivyosema kwamba:

Katika nyaraka za Paulo "*... yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe. Basi, wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu, mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu.*" 1 Petro 3:16-17

18. Petro ametuonya kwamba watu wengi huelewa vibaya maneno ya nani? __________________

Basi, bila shaka maneno ya Paulo yafuatayo ni miongoni mwa yale ambayo watu hushindwa kuyaelewa. Twasoma:

"*Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo. Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima. Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu*

*wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki.*" Warumi 5:17-19

Basi, kusudi tuelewe maneno hayo ya Paulo, tunaweza kukumbuka tena mfano wa watu waliopanda basi. Dreva wa gari hilo alikuwa akiwasimamia watu wote waliokuwa ndani ya gari pamoja naye. Kwa hiyo, magari yalipogongana, hata watu waliopanda basi waliweza kusema "tumegongana" kana kwamba wameshiriki kosa la dreva. Walakini, twajua kwamba mwenye hatia ni dreva peke yake. Vivyo hivyo, Adamu ametusimamia wanadamu wote, maana tulikuwa ndani ya mwili wake. Kwa hiyo, inaweza kusemwa kwamba wanadamu wote tumetenda dhamnbi katika Adamu, hata ingawa hatuna hatia ya dha mbi yake. Hivyo, miili yetu hufa lakini roho zetu hazitahukumiwa kwa kosa lake.

Kumbuka, Mungu ambaye hawezi kusema uongo ametuambia "*Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa. Mwana hatauchukua uovu wa baba yake*." (Ezekieli 18:20).

19. Miili yetu hufa kwa ajili ya dhambi ya Adamu, walakini roho zetu zitakufa kwa ajili ya dhambi ya nani? ____________________

**YESU NI MKOMBOZI WA WENYE DHAMBI**

Inafaa sana kwamba mwanafunzi akumbuke jinsi Yesu anavyoitwa Mkombozi. Kwa nini Yesu huitwa hivyo? Kusudi tupate kujibu swali hili inatakiwa tufahamu kwanza maana ya kukombolewa. Basi, tutoe mfano.

Hapo zamnani, mtu fulani alipatwa na tatizo kubwa akihitaji fedha. Kwa hiyo, alichukua redio yake akaipeleka kwa mtu mwenye kuwakopesha watu fedha. Yule mkopeshaji alikubali kuirudisha redio wakati mwenye shida atakapoikomboa kwa kulipa deni yake. Hivyo twaona kwamnba mkombozi maana yake ni mtu ambaye ananunua tena mali yake nwenyewe iliyoachwa kwa mtu mwingine. Basi, kwa kuwa Yesu ni mkombozi wetu, <u>twatambua kwamba tuliwahi kuwa mali yake</u>. Halafu tulifanywa kuwa mali ya mtu mwingine. Kisha tulinunuliwa (yaani, tulikombolewa) tuwe mali ya Yesu tena! Biblia huonyesha kwamba mtoto anapozaliwa huitwa mtoto wa Mungu. Walakini, mtoto akifika makamu ya kutambua mema na mabaya, huanza kutenda dhambi na kuhesabiwa kuwa mtoto wa Ibilisi (yaani, Shetani), Twasoma:

"*Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki; atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo… Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao, Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake.*" 1 Yohana 3:7-8,10

Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao nauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki." Warumi 6:16

"*Naye (Mungu) alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye <u>katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi</u>.*" Wakolosai 1:13-14

"*Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo.*" 1 Petro 1:18-19

20. Hapo juu tumethibitisha kwamba watoto hawarithi dhambi bali ni wenye haki. Kwa hiyo, watoto wachanga huhesabiwa kuwa watoto wa nani? ___________________

21. Mtoto wa makamu anapoanza kutenda dhambi hujifanya kuwa mali ya nani?

___________________

22. Kwa hiyo, mwenye dhambi huhitaji kukombolewa awe mali ya Mungu tena. Katika Yesu tunao ukombozi, yaani, msamaha wa nini? ___________________

**WATOTO WACHANGA WASIBATIZWE**

Watoto wachanga hawana haja ya kukombolewa na Yesu kwa sababu wao ni mali yake tayari. Tena, hawana haja ya kubatizwa kwa sababu hawana dhambi. (Kusudi la kubatizwa ni kuondoa dhambi, Matendo 2:38; 22:16). Ebu! tuthibitishe jambo hili kwa maneno ya Yesu mwenyewe:

"*Basi wakamletea watoto wadogo ili awaguse; wanafunzi wake, wakawakemea. Ila Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia, Waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. Amin, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa. Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabarikia.*"

Marko 10:13-16

23. Watoto hawakuletwa kwa Yesu ili awabatize bali walileletwa kusudi afanye nini?

___________________

24. Yesu alisema kwamba watoto wadogo hustahili kuingia wapi? ___________________

25. Je! ikiwa watoto hawa wangalikuwa wenye dhambi Yesu angaliweza kusema kwamba ufalme ni wao? (1 Wakorintho 6:9-10) ___________________

26. Yesu alisema kwamba watu wakubwa hawataingia katika ufalme wasipoukubali kama nani?

___________________

27. Je! ikiwa watoto wadogo wangekuwa wenye dhambi, Yesu angetuambia kufananishwa nao?

___________________

28. Yesu hakuwabatiza watoto, bali aliwakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, halafu akafanya nini? ___________________

Katika Biblia huwezi kusoma habari ya mtoto mchanga ye yote aliyebatizwa. La! bali twasoma:

"*Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo… Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake.*" Matendo 8:5,12

29. Je! Filipo aliwabatiza watoto wachanga? __________________

Mtoto mchanga hawezi kubatizwa kwa sababu hawezi kutii amri ya Yesu ifuatayo:

"*Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*" Marko 16:16

30. Je! mtoto mchanga aweza kuamini? __________________

Baadhi ya watu hudhani kwamba mtoto mchanga anaweza kubatizwa kwa imani ya wazazi wake. Jambo hili si kweli. Kumbuka Yesu alisema "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka.*" Kwa hiyo, mtu hawezi kuokolewa kwa imani ya mwenzake. La! bali twasoma:

"*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Waebrania 11:6

"*Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe; haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake.*" Ezekieli 18:20

Kumbuka pia kwamba kila mtu atapokea ujira wa matendo yake mwenyewe, siyo kwa ajili ya matendo au imani ya mwenzake. Twasoma:

"*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya.*"
2 Wakorintho 5:10

31. Je! mtoto aweza kubatizwa na kuokolewa kwa imani ya baba yake? __________________

Kama tulivyothibitisha huko juu, mtoto mchanga hana haja ya kuba tizwa kwa sababu yeye hana dhambi. Tena, mtoto mchanga hana haja ya kukombolewa kwa sababu yeye ni mtoto wa Mungu. Yesu alisema, watoto wachanga ufalme wa Mungu ni wao. Kwa hiyo, mtoto akifa angali mchanga, basi atakwenda kwa Mungu tu hata ingawa hajabatizwa.

Watu ambao wanaamuru watoto wachanga wabatizwe wako katika hatari kubwa; maana, twasomna:

"*Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze, mpate kuzishika amri za Bwana, Mungu wenu, niwaamuruzo.*" Kumbukumbu 4:2

"*Usiongeze neno katika maneno yake; asije akakulaumu ukaonekana u mwongo.*" Mithali 30:6

"*… Wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi* (mitume) *au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.*"
Wagalatia 1:7-8

“*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki.*” Ufunuo 22:18

32. Je! Mungu amewaamuru watoto wachanga wabatizwe? ___________________

33. Je! viongozi wa dini wanaofunga amri hizo za kuwabatiza watoto wanatusaidia au wanatutaabisha? ___________________

34. Mwisho wao utakuaje? ___________________

************************************************************************************

Jina lako ………………………………………………
Anwani yako ……………………………………………

## ***KANISA la KRISTO***

## ***Tanzania***